



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA AMANI MKOA WA MJINI MAGHARIBI TANZANIA ZANZIBAR PAMOJA NA UDIWANI KATA SABA (7) TANZANIA BARA TAREHE 17 DESEMBA, 2022

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Jimbo la amani Mkoa wa Mjini Magharibi Tanzania Zanzibar pamoja na Udiwani Kata Saba (7) Tanzania Bara kuwa kutakuwa na **Uchaguzi Mdogo wa Ubunge na Udiwani siku ya Jumamosi, tarehe 17 Desemba, 2022**. Kata zitakazofanya Uchaguzi ni Majohe (Dar es Salaam CC) Dar es Salaam, Mndumbwe (Tandahimba) Mtwara, Njombe Mjini (Njombe TC) Njombe, Dunda (Bagamoyo DC) Pwani, Mwamalili (Shinyanga MC) Shinyanga, Mnyanjani (Tanga CC) Tanga, na Vibaoni (Handeni DC). Tanga.

Upigaji Kura utafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Vituo vitafunguliwa saa moja kamili (1:00) Asubuhi na kufungwa saa kumi kamili (10:00) jioni. Utaratibu utakaofuatwa siku ya Uchaguzi ni kama ifuatavyo:-

1. **SIKU:** Wananchi watapiga Kura siku ya Jumamosi tarehe 17 Desemba, 2022
2. **VITUO:** Upigaji kura utafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 1:00 kamili Asubuhi na kufungwa saa 10:00 kamili Jioni

Mambo ya kuzingatia wakati wa Uchaguzi

1. Mpiga Kura anatakiwa kutunza kadi yake ya kupigia kura aliyoitumia kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na kuhakikisha anakwenda nayo kituoni siku ya uchaguzi.
 2. Aidha, kwa Kata saba (7) Tanzania Bara, Wapiga Kura waliopoteza kadi zao za kupigia kura au zilizoharibika, wanaruhusiwa kutumia mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo:-
 - Hati ya kusafiria,
 - Leseni ya Udereva na,
 - Kitambulisho cha Uraia ambacho majina yote matatu yafanane na yaliyomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura
 3. Kwa Upande wa Jimbo la amani Mkoa wa Mjini Magharibi Tanzania Zanzibar, watakaruhusiwa kupiga kura ni wale walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).
 4. Mpiga Kura anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni ambapo kutakuwa na mstari wa wanaume na wanawake.
 5. Mpiga Kura awapo kituoni anatakiwa kutoa kipaumbele kwa Wapiga Kura wenye mahitaji maalumu kama vile Wazee, Wagonjwa, Watu Wenye Ulemavu, wajawazito na wenye watoto wachanga (watakaokuwa nao kituoni).
 6. Ifikapo muda wa kufunga kituo saa 10:00 kamili Jioni kama Wapiga Kura bado wapo kwenye mstari, Mlinzi wa Kituo atasimama nyuma ya mtu wa mwisho na zoezi la upigaji kura litaendelea hadi wote wanamalizika. Mpiga Kura atakayefika zaidi ya muda wa kufunga kituo hataruhusiwa kupiga Kura.
 7. Mpiga Kura anatakiwa afuate maelekezo yote atakayopewa na Msimamizi wa Kituo.
 8. Baada ya kumaliza kupiga kura, Mpiga Kura anatakiwa kuondoka eneo la kituo cha kupigia kura.
- Kumbuka kuzingatia kanuni za afya kwa kufuata maelekezo utakayopewa kituoni ili kujiepusha na maambukizi ya ugonjwa wa Ebola na UVIKO-19 unaosababishwa na virusi vya korona.

Dkt. Wilson Mahera Charles
MKURUGENZI WA UCHAGUZI

Tangazo hili limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Eneo la Uwekezaji Njedengwa, Kitalu D, Kiwanja Na. 4, Uchaguzi House, S. L. P. 358, Dodoma. Barua Pepe: uchaguzi@nec.go.tz
info@nec.go.tz. Tovuti: www.nec.go.tz.